HII NDIYO ZAWADI

Martin M. Munywoki,
Sep 17, 2017
Nairobi.



MASHAIRI



HII NDIYO ZAWADI

{ Hii ndiyo zawadi ya leo, niliyoandaa (kukupa)
Ikubali (ikupendeze), ipokee (ikupendeze),
Itakase, (na mimi Bwana) na unibariki } *2

1. Japo haitoshi, haipendezeshi, ndilo jasho langu, la mikono yangu,
   Japo ndogo sana, ipokee Bwana, hii niletayo, kutoka kwa moyo!

2. Japo kila saa, nakutegemea, unipe unipe, husemi nilipe,
   Nikikulilia, unanisikia, nikipungukiwa, wanizidishia!

3. Japo sistahili, unanikubali, kwa hali na mali, unanifahili,
   Ndipo naja mbele, na zawadi tele, niziweke pale, ulipo milele!